# *KUHESABU KINYUMENYUME*

Asante. Asante, Ndugu Moore. Mwaweza kuketi. (Hiyo ni sawa, ndugu, iwashe.) Asante kwa mwaliko. Inaonyesha kwamba watu bado wana njaa, jinsi ninavyozungumza na kupiga makelele; na bado mnaendelea kurudi. Kwa hiyo ninawashukuru. Bwana awabariki daima ndilo ombi langu.

2 Huu umekuwa wakati mmoja mtukufu kwangu. Nimeufurahia kweli, nilikuwa na wakati mzuri sana, wakati wa ajabu wa ushirika kwenye Neno na mambo ya Mungu.

3 Nimekuwa nikishangaa. Huyu siye Dada Lyle, sivyo, anayeketi hapa? Mnajua, hivi majuzi usiku nilizungumza kuhusu mume wako huko Azusa, kuhusu mkutano wa Mtaa wa Azusa, ndipo—ndipo nikatazama pande zote nikakuona, nilifikiri ungekuwa mkongwe kuliko hivyo, kwa hiyo mimi... Kisha nikagundua, nami...Dada Moore, niliona picha yake... Kitabu kile ulichoandika, ninacho. Ni kizuri sana. Na kwa kweli kilikuwa kinanirejesha kwenye siku za kale, uliposema ulivaa...kuvaa gauni hilo moja kwa muda mrefu sana, ama chochote kile. Na maskini Dada Moore, aliye hapa, maskini jamaa aliyevaa nguo za mitumba, alifurahia tu kuwa pamoja nanyi.

4 Dada Moore, nafikiri umeunganishwa nao Milele. Wakati maisha haya yatakapokwisha, na yale maisha ng'ambo ya pili, ile duara kuu ya familia ha—haitavunjika. Ulikuwa na mapambano mengi sana na kadhalika katika maisha haya, lakini maisha hayo yajayo, yatakuwa bora zaidi. Tunajua kwamba mapambano yamekwisha. Mungu awabariki nyote.

5 Anna Jeanne, bado sijaona kofia hiyo ya mtoto, lakini mimi...Ni wangapi walifurahia makala hiyo? Hiyo ilikuwa nzuri kweli. Mimi...Mimi na mke wangu, tulikuwa na wakati mzuri tu. Kwa hivyo Billy ana picha zao zote mle, zile...

6 Naye Jackie? Hivi yeye—yeye hayuko hapa? Nilimwona yule mvulana wake mdogo. Kama akiendelea kukua, ataenda kuwinda dubu kwa ngumi zake. Yeye—yeye ni jamaa mkubwa mno, sivyo? Yeye—yeye kweli ni kama mwanamume mdogo. Nasi tunafurahi sana kuwaona vijana hawa, na kuwaona wa—watu wazima wangali wameshikilia, vijana wakija.

7 Asubuhi ya leo sikuwa na wakati wa kutambua kila mtu anayetoka...niliyemjua kutoka maskanini, na ujirani. Si—sikatai. Baadhi ya watu, nami...Mnaelewa, nina hakika. Sasa, kwenu mnaotoka maskanini, tutawajulisha haraka iwezekanavyo kama tunaweza kufanya maandalizi kwa ajili ya zile Nyakati Saba za Kanisa, zikifuatiliwa na ile Mihuri Saba ya Mwisho.

8 Sijui. Huenda ikanibidi kushuka, nichunge Maskani yangu hapa chini. Hawataniruhusu nijenge chochote juu ya hiyo kule, watu wa kugawa maeneo. Na kwa hiyo, si—sijui tutafanya nini. Kabisa hawaniruhusu—inaonekana hawataki nijenge. Na kwa hiyo, tumekuwa tukilipigania kwa muda mrefu, wala hatuwezi kujenga. Kwa hiyo, lakini tutaendelea na kulitumia hili hata hivyo, labda, kabla hakujaingia baridi sana.

9 Sasa, kumbukeni, mara ya kwanza nilipowaacha nyote hapa Shreveport, nilitoa tamshi hivi: Kama ninaweza kuwafadhili kamwe (Mnaona?), usiku hautakuwa giza kupita kiasi; mvua haitanyesha kupita kiasi. Kwa hiyo kumbukeni tu, hiyo bado ingali iko. Nipigieni simu wakati wowote. Chochote ninachoweza kufanya, nitafurahia kukifanya.

10 Wakati mwingine katika kukemea katika Injili (Mnaona?), na mambo kama hayo, si kwa sababu kwamba siwapendi; nawapenda. Mnajua, si vizuri kufanya mizaha midogo, lakini, kubadilisha hicho kitu, kama yule mvulana mdogo aliyekuwa akichapwa, mwajua, naye baba yake akasema, "Mwanangu, hii itanidhuru kuliko inavyokudhuru wewe."

Akasema, "Baba, nina hakika hutanichapa basi."

11 Hi—hivyo mimi. . . Lakini mijeledi ya Injili ni tofauti. Haipendezi sana kuitumia, lakini hata hivyo, ndiyo mambo tunayohitaji. Basi tunaamini kwamba Mungu atawabariki sana. Ninaomba maombi yenu sasa, na nikiwa ng'ambo. . .

12 Sasa, Ndugu Jack alikuwa akiniambia huko nje ya kwamba walitoa ma—matoleo ya upendo kwangu. Na kwa hiyo sikutaka hivyo. Lakini nilitaka kumzuia. Nilifikiri angefanya hivyo usiku wa leo, lakini alikuwa tayari amefanya, usiku, wakati fulani hapo kabla. Kwa hivyo yatageuzwa kwa kazi ya umishenari kupitia kwa maskani. Siyapati moja kwa moja mimi. Yanaingia kwenye maskani, na ndipo itakuwa. . . kusaidia kutuma huko ng'ambo mahali ambapo hawawezi kulipia Injili na kufanya mikutano. Kisha akiba hiyo. . .

13 Maskani haiitumii kwa ajili yao wenyewe. Hao hapo wadhamini wameketi papa hapa sasa. Mnaona? Hivyo wao—wao hawayatumii kwa ajili yao wenyewe. Yanaingia kwenye uamsho, moja kwa moja kwenye uamsho. Ila tu wao ni wakfu. Mnaona? Na kwa hivyo yatatumika kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

14 Hata sininii—hata sana sana siidhinishi hiyo hundi. Hata hupigwa muhuri, ikawekwa benki, na kuhifadhiwa kwa ajili ya hazina hizi kwa ajili ya miamsho hii, na hiyo pekee (Mnaona?), kwa ajili ya Injili ambayo mmekuwa mkiisikia, ili kuienezea watu ambao hawana uwezo wa kukodisha uwanja wa michezo au mahali pa kuifanyia.

15 Halafu, kwa ajili ya kuwatembelea wagonjwa. Hakuna mtu. . . Maskini, kundi la watoto wadogo huko nje wasio na chochote, hakuna njia ya kukufikisha huko. Na kwamba, kama

ikibidi niende kuchukua tikiti ya ndege, wananinunulia nami naenda huko na kutimiza wito huo, na kumwombea maskini mtoto huyo mgonjwa, hata aweje, kisha narudi, huko ndiko pesa zenu zinakoenda. Hivyo ndivyo zinavyotumika, maana sina budi kuziwajibikia huko juu. Mnaona? Mnaziaminia kwangu, nami sina budi kuwa msimamizi Wake. Nataka nipatikane sina hatia ya jambo lolote baya kwa njia hiyo. Mungu awabariki. Sasa, hebu na tuinamishe vichwa vyetu kidogo tu kwa ajili ya maombi.

16 Baba yetu wa Mbinguni, Ee Mungu, si zaidi ya dakika kumi zilizopita, nikiona ono hilo likitokea kwenye dawati hilo kwa maskini mama mzuri hapa nyuma; najua imekwisha sasa. Ninashukuru sana kwamba Wewe ni Mungu. Ninashukuru sana kwamba tuna Mtu ambaye tunapoweza kuja kwake, nalo lika-. . .likatatuliwa vizuri. Tunakushukuru kwa yote ambayo umetufanyia.

Tunakushukuru kwa ajili ya watu hapa Shreveport, na Texas, na kote katika majimbo ambao wamekusanyika kwenye mkutano huu.

17 Bwana Yesu, utusamehe nji—njia zetu, ambazo labda tunashindwa mahali fulani, labda kupata ujumbe jinsi inavyopaswa kuwa. Lakini, Baba, ninaomba kwamba mahali ambapo tumekosea, kwamba Roho Mtakatifu mkuu atayachukua haya maneno, na kuyageuza, na kuyaweka mioyoni mwao kwa njia iliyo sawa, ili waelewe kwamba ni wakati wa maandalizi sasa kabla ya kuondoka kwa kanisa.

18 Jalia sote tuishi kwa ajili ya saa hiyo, Bwana, tuishi leo kana kwamba inaweza kuwa ni leo. Na endapo hayupo hapa leo, tutakuwa tukimtazamia kesho. Dumisha mioyo yetu ikiwa safi kutokana na dhambi na ubinafsi. Dumisha mioyo yetu safi, nafsi zetu zisiwe na taka, kwa Damu ya Yesu Kristo, tupate kutembea pamoja Naye na kuishi pamoja Naye milele.

19 Mbariki Ndugu Jack Moore, Ndugu Lyle, Ndugu Brown, ndugu hawa wote wema, Bwana, wafanyakazi wao hapa. Walei hawa hapa nje, jinsi mwaka baada ya mwaka wao. . .tunaketi pamoja mahali pa Mbinguni, na kuyajadili Maandiko, na kuwa na nyakati za ajabu za ushirika. Mbariki Dada Moore, Anna Jeanne, Dada Lyle, wanawake hawa wazuri wote, Bwana, kila mmoja wao. Ninaomba baraka Zako. . .Kwaya hii ndogo ya kupendeza. . .Utubariki tu pamoja, Baba.

20 Tunakupenda, na tunakuomba utusamehe makosa yetu na utujalie kwa uwezo Wako mkuu, ili tuwe mashahidi katika sehemu ya dunia ambayo tunapaswa kuingia, popote utakapotuita. Katika Jina lake Yesu Kristo, tunaomba. Amina.

21 Sasa, usiku wa kufunga huu uamsho, nami nimekuwa nikiwaweka kwa muda mrefu kila usiku. Kwe—kweli nitajaribu nisifanye hivyo usiku wa leo, kwa sababu kesho mtaenda kazini, nami sina budi kuamka. Nikiisha kufika nyu-. . .huko kwangu

na kufunga virago, nami nina kama maili mia saba na hamsini za kuendesha gari kutoka yapata saa nane na nusu usiku. Sina budi kuwa Jeffersonville, kwa yote yawezekanayo, Bwana akipenda, kwa miadi kesho usiku.

22 Kwa hiyo, nami nimechoka, nimechoka. Ninaenda tu mahali mahali. Na—na hivyo mimi . . . Lakini ninapoanza kula Mana hii ya Mbinguni, ni—nina ninii tu, nina, nina uwezo mkubwa tu, na huruma kubwa, kwa ajili ya wengine.

23 Kwa hiyo ninawatakeni mfungue usiku wa leo kifungu kimoja katika Maandiko yanayopatikana katika Kitabu cha Waebrania. Huo ndio waraka ambao tunaamini kwamba Paulo aliuandikia Waebrania, akitenganisha torati na neema.

24 Na halafu nafikiri ya kwamba Billy alisema jana usiku alisambaza kadi za maombi. Na dada mmoja hapa nyuma muda mfupi uliopita, huku amemshika mtoto Kasisi Price, mwenye umri wa kama majuma matatu ama manne, ama, mwenye umri wa miezi kadhaa, ama, umri wa majuma kadhaa, naamini ndivyo, aliyeketi kule nyuma, alisema mumewe ataninii, alitaka kuombewa. Na hiyo ndiyo sababu . . . Nasikia alisema, "Lakini ana kadi."

Nikasema, "Vema, sawa. Basi nitamaliza kwa wakati mzuri, ili niweze kuziita kadi hizo za maombi, na kuwaombea wagonjwa."

25 Sasa, kumbukeni, katika kuwaombea wagonjwa, unajitia nanga kwamba maombi ya imani yamekuwa—yamefanywa kwa ajili yako. Wala usitilie shaka hata kidogo, amini tu kwamba ndivyo ilivyo, na itatimia.

26 Sasa, ninaamini kama sisi, kama watu, tuna uthibitisho mkamilifu, mkamilifu kabisa ya kwamba Yesu Kristo yu pamoja nasi. Je, unaamini hilo? Yesu Kristo yu pamoja nasi. Na kwa hiyo kama yuko hapa, Yeye yuko hapa kujibu na kutuhudumia kila baraka aliyoahidi katika Neno.

27 Kwa hiyo tunapoomba na kuweka mikono juu ya wagonjwa, tunawatarajia muamini jambo hilo. Mungu anawatarajia muamini hilo. Kamwe msiliondokee. Msiruhusu chochote kiwatikise.

28 Kama nilivyomwambia muda mfupi uliopita . . . yule msichana, "Pigilia tu nguzo hapo niani mwako, 'Katika jukwaa hili usiku wa leo maombi ya imani yaliombwa kwa ajili yangu. Pia, Shetani, Damu iliwekwa kati yangu na wewe. Kwa hiyo afadhali uondoke.'"

Unaweza kuja kufikia nguzo hiyo, na kusema, "Uh-uh." Hii hapa dalili, unasema . . .

29 Usiipige ngumi. Usimpige ngumi, kumpiga nyoka, endelea tu kusema, "Nakukemea. Na- . . . " Atakuuma. Unaona? Mpuuze tu, mwondokee. Kwa hiyo, ameshindwa kwa vyovyote vile, kwa

hiyo, haya basi. Unaona? Kamwe usi—usimpige ngumi, useme, “Ee Bwana, mkemee, mkemee.” Uh-uh. Usifanye hivyo. Unaona? Unadhoofisha kile unachoamini kweli. Unaona, unaona?

30 Wewe amini la sivyo usije huku. Ukija, basi amini, na uache hilo litoshe. Ni hayo—ni hayo tu. Unaona? Simama tu papo hapo na useme, “Imekwisha. Ni hayo tu. Hilo latosha.”

Sasa, nitakaporudi huku tena, nitashuka labda kuja kufanya uamsho wa uponyaji na sio mkutano, na tutazungumza sana juu ya uponyaji wa Kiungu.

31 Sasa, katika Waebrania 11, kama kila mtu ameipata, mlango wa 11, na kifungu cha 3, ningependa kusoma, kutoa katika somo hili la Maandiko haya muktadha wa kusoma, au, kifungu.

> *Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri.*

32 Maandiko ya kipekee sana, sivyo? Lakini kutokana na haya nataka kuzungumza juu namna fulani ya jambo la kisasa. Ninataka kuchukua kitu ambacho ni cha kisasa, na kukilinganisha na cha kale, kwa sababu mambo yote katika Biblia, ama yaliyokuwako, ni mfano wa mambo yajayo.

33 Sasa, somo langu usiku wa leo linaitwa, “Kuhesabu Kinyumenyume.” Sasa, mambo. . .vitu vyote katika maumbile ni mifano ya vitu vya kiroho. Tunaelewa hilo. Mnaona? Ya asili ni mfano tu wa ya kiroho.

34 Ninaamini katika mageuzi yanayoendelea, lakini si jinsi wanasayansi walivyosema yanakuja. Na tayari wamejishinda wenyewe juu ya hilo. Wakati wanafikiri ya kwamba *kitu fulani* kilizaa *kitu fulani*, na *hiki* kilifanya *hivi*, nacho kikageuka, la, bwana.

35 Roho Mtakatifu mkuu alianza kuatamia juu ya nchi, ndipo ukaja aina moja ya uhai, kisha aina nyingine ya uhai. Nao ukaendelea kupanda juu, kupanda juu, kupanda juu mpaka ukafikia sura hasa ya Yule aliyekuwa akiuatamia: sura ya mwanadamu. Ilithibitika, wakati Mungu alipofanyika mwili, Yeye alikuwa Mwanadamu. Kamwe hakikutoa kitu chochote kikubwa zaidi, maana haiwezekani. Muumba Mwenyewe alikuwa ni Mwanadamu. Mnaona?

36 Sasa, na kisha, mbona, unautazama mti, jinsi unavyopendeza, jinsi ulivyo na madaha. Je, mti huo unawakilisha nini? Mti wa Uzima. Mnaona? Kuna kitu mbinguni cha kuuwakilisha. Mnaona? Na hiki ni kivuli tu cha vitu vilivyo halisi. Huu ni upande hasi.

37 Tunapotaka kuishi, madaktari, kila mtu anafanya kazi kimwili, kujaribu kuishi. Ni kwa nini? Kwa sababu ni uhai. Na inawakilisha tu, na inaonyesha, ya kwamba, upo mwili ambao hauwezi kuugua, na ambao hauwezi kufa. Huu hapa unaoweza

kufa unathibitisha tu kwamba kunao usioweza kufa. M—mti unaokufa unathibitisha kwamba kuna mmoja usioweza kufa, kwa maana ni kivuli cha mambo yatakayokuja katika maumbile. Masomo makubwa katika miti, mimi huutazama mti.

38 Hapa, si muda mrefu uliopita, mama yangu alipokuwa mahututi na alikuwa yuafa, basi Delores aliniita (na ndiyo kwanza ampokee Roho Mtakatifu hivi majuzi), kwa hivyo akasema, “Bill, mimi,” (yeye ndiye mtoto) basi akasema, “Siwezi kuvumilia, Bill,” kisha akasema, “Mama, Mama yetu wa pekee. . . ”

Nami nikasema, “Kwa nini . . . ”

Akasema, “Mungu angewezaje . . . ”

39 Nikasema, “Masalale, ngoja kidogo (Um-hum.) hebu kidogo.” Nikasema, “Biblia ilisema, ‘Ina thamani machoni pa Bwana mauti ya watakatifu Wake.’” Nikasema, “Mwangalie yule mzee wetu amelala pale kwenye kitanda kile, akiendelea kutabasamu tu, na kumwita Bwana Yesu, hakuna kitu kinachomgusa.” Nikasema, “Bado ninaweza kumwona wakati aliponikumbatia, nami nilikuwa mvulana mdogo tu, na kumbatiza katika Jina la Yesu Kristo, huko nje mtoni, nikamwona Roho Mtakatifu akimjilia.” Nikasema, “Mbona, hakika, ameenda, anaenda kukutana na baba.”

Kasema, “Kweli mimi, Bill, siwezi kuvumilia.”

Nikasema, “Delores, kuna mwaloni kushoto kwa dirisha lako.”

Akasema, “Ndiyo.”

Nikasema, “Majira yote ya kiangazi, si umekuwa mzuri na hayo majani ya kijani kibichi?”

“Ndiyo.”

Nikasema, “Yakoje sasa?

Akasema, “Naam, ni ya kahawia, manjano, kijani kibichi.”

“Um-hum,” nikasema, “ni lini yalikuwa ya kupendeza zaidi? Yalipokuwa kijani, au mahali yalipo sasa?”

Akasema, “Sasa.”

Nami nikasema, “Ingawa yanakufa. Hapo ndipo maisha yanapendeza zaidi.” Um-hum. Hiyo ni kweli.

Alipofikia mahali . . . Nikamwambia, nikasema, “Mama, unajisikiaje sasa?”

Akasema, “Vizuri sana.”

40 Alipofika mahali asingeweza kuongea tena, nikasema, “Mama, mimi ningali ni mvulana wako mhubiri, Billy. Je, unanitambua?” Asingeweza kuzungumza tena. Nikasema, “Ikiwa Yesu angali ana maana kubwa kwako kadiri alivyokuwa

siku ile ulipompokea katika umbo la Roho Mtakatifu, pepesa macho yako upesi sana."

Naye akapepesa macho yake, huku machozi yakitiririka mashavuni mwake.

Ndipo upepo kidogo ukaingia chumbani naye akaondoka nao. Loo, naam. Mnaona? Ni sawa.

41 Mti huning'iniza jani lake. Na muda si muda mwajua, jani hilo huanza kubadilisha rangi wakati uhai unapoliacha. Inakuwaje? Ni. . . Uhai ulio ndani ya jani unarudi tena kwenye shina la mti ambamo ulitoka, kisha unarudi tena katika majira ya kuchipua kuleta jani jingine.

42 Nasi tuko kwenye Mti wa Uzima tunapozaliwa mara ya pili. Ndipo uhai unapouacha huu, huo uhai unamrudia Mungu aliyeutoa, upate kurudi tena katika ule Utawala wa Miaka Elfu Moja pamoja na jani lisiloweza kupukutika kutoka mtini. Um-hum, um-hum. Amina. Haya basi, Milele. Hayo ni maisha ya kudumu; tunao Uzima wa Milele. Mnaona? Yanaanguka, yanachipuka. Ni kitu gani? Mambo ya asili yakiwa ni mfano wa ya kiroho.

43 Hebu angalia mwili huu hapa, miili yetu ni kipeo cha jinsi gani. Hakuna kitu kama hiyo. Hakuna kitu kilichowahi kupatikana kingeweza kuchukua mahali pake, hisia na kadhalika. Ni kitu kikuu jinsi gani: viganja, mikono, pua, kinywa, kila kitu kama tu tunavyovihitaji. Ni jambo kubwa. Ni nini? Mwili wa kawaida ni mfano wa mwili wa kiroho, "Kwa maana maskani hii iliyo ya dunia ikiharibiwa," tuna nyumba nyingine ya kuhamia. Mnaona? Hii ni kivuli tu cha ile ijayo.

44 Tunawazia bibi na bwana arusi. Ilitokea tu niliangalia kwenye baadhi ya vijana, wanaotaka kufunga ndoa, kwa hiyo nilikuwa nikiwazia juu ya bibi na bwana arusi. Vema. Hao ni mfano wa nini? Ya kimwili ni mfano wa ya kiroho, Bibi na Bwana-arusi. Hiyo ni kweli.

Vitu vyote—vitu vilifanywa kwa vitu visivyoonekana. Sasa, angalieni. Sikuzote ni kufananisha: mwili wa kiroho, mwili wa kawaida.

45 Na sasa, tunaishi hapa, ambapo kile tunachoamini kipo, kuna hisi sita, hisi tano, hasa, lakini imani hufanya hisi ya sita. Sasa, nasi tunaishi, sasa humu ndani, kile tunachowazia, tunachoita, "viwango vitatu." Huenda nisivitaje sawa sawa. Nadhani hivyo viwango vitatu vinaitwa (Baadhi yenu ninyi watoto kutoka shule ya upili mnaweza kunisahihisha juu ya hili.) mwanga, hewa, na wazo: viwango vitatu. Sasa, au, hiyo ni kweli? Mwanga, hewa, na wazo. Hivyo ndivyo vile viwango vitatu, sivyo? Nafikiri hiyo ni kweli. Vema.

46 Sasa, tuna, tunajua, kuna kiwango kingine, ambacho ni kiwango cha nne, kwa sababu sayansi imekichunguza

na kukipata, nacho ni redio. Hakuna hisia za mwili wetu zinazoweza kutambua redio au televisheni juu ya wimbi hilo la etha. Hata hivyo moja kwa moja kupitia kwetu sasa kuna sauti za watu zinazokuja. Moja kwa moja kupitia hapa zinakuja picha za televisheni. Lakini hatuna chochote ndani yetu, hakuna njia kabisa ya kuwasiliana nazo ndani yetu. Inahitaji fuwele ya aina fulani, au sumaku, kuwasiliana na hizo. Lakini inasema kwamba kuna kiwango kingine. Sasa, hivyo ni viwango vinne.

47 Basi, nadhani kiwango cha tano ni pale mwenye dhambi anapokufa, mahali aendapo. Sasa, nafikiri kwamba mwenye dhambi anapokufa huenda kwenye kiwango hiki cha nne. Angalieni. Jambo la kwanza, hawezi kwenda Mbele za Mungu kwa sababu yeye ni mwenye dhambi, nao wakati wake umekwisha duniani.

48 Kama ningeufananisha kwenu, ni kama kujaribu kulala nawe uko kwenye. . .huwezi kulala, nawe uko kwenye jinamizi. Wewe. . .Mambo ya kutisha, unapiga mayowe. Kabisa wewe. . . Hiyo ndiyo hali ya waovu waliokufa. Hawezi kwenda katika Uwepo wa Mungu kwa sababu yeye ni mwenye dhambi. Hawezi kurudi duniani kwa sababu wakati wake umekwisha. Naye amenaswa kati ya vitu hivyo viwili katika kiwango cha tano. Yeye ana nafsi, nayo haiwezi kwenda Mbele za Mungu, kwa maana haijafunikwa na Damu. Yeye ni mwenye dhambi. Hawezi kujiamsha mwenyewe, kwa sababu wakati wake umekwisha duniani. Kwa hiyo yeye huyo hapo, katika jinamizi la mateso.

Wazia hilo sasa, kabla hujaingia: jinamizi, kupiga makelele.

49 Wengi wetu tumekuwa na jinamizi. Ni kwa sababu, tunaambiwa, kwa sababu dhamira mbili zinapita, dhamira ya ndani na ya kwanza, nazo zinashikania katikati, na hiyo ndiyo jinamizi. Basi wakati mwenye dhambi anapokufa, anashikwa huku nafsi yake iko kati ya dunia na kuzimu katika jinamizi, huyo hapo amesimama.

50 Sasa, kiwango cha sita ni katika Kristo, watakatifu, watakatifu waliokufa, ama, watakatifu waliopumzika, ambao kabisa, kazi imekamilika duniani, nao wameingia kwenye raha pamoja na Kristo chini ya madhabahu, vizuri. Kama ungeilinganisha na ndoto nzuri ambapo hukutaka kuamka. Si ndoto, ni maumbile. Ni halisi. Lakini ninawatoleeni mfano tu. Na bila shaka, kiwango cha saba ni Mungu peke yake.

51 Sasa, angalieni matukio ya kisasa tuliyo nayo. Tunaangalia wakati huu wa kisayansi tunaoishi, wakati wa kubonyeza kitufe. Na hata hivyo, watu wana muda mfupi wa kuomba kuliko waliowahi kuwa nao, katika nyakati hizi zote za kisasa. Walikuwa wakiketi usiku kucha, wakisikiliza mahubiri. Na sasa kabisa hatuwezi kufanya hivyo. Hatuna wakati wa kufanya hivyo. Mnaona, liko tu kichwani mwetu. Tunafikiri hatuna muda wa kulifanya, lakini tunao.

52 Lakini matukio ya kisasa ni mtangulizi wa matukio ya kiroho. Sasa, kumbukeni, matukio ya kisasa ni watangulizi wa matukio ya kiroho, ya kawaida kama ya kiroho, hasa. Kila matukio huambatana na mengine, ila tu limeboreshwa kuliko hilo lingine. Kila kitu kinachotokea katika mambo ya kawaida, basi kitu kingine kinachotokea kimeboreshwa zaidi.

53 Kwa mfano, hebu tuchukue, kwa mfano, sasa, usafirishaji. Siku moja kulikuwa na farasi na mkokoteni, kisha tukapata motokaa. Hizo zingali ni nguvu za farasi, lakini ni nyingi zaidi katika motokaa. Ilikuwa ni uboreshaji wa nguvu za farasi. Bila shaka. Tulipopata motokaa, ilikuwa ni bora kuliko farasi na mkokoteni. Ndipo basi tukaendesha farasi na mkokoteni. Kisha tukachukua motokaa. Na baada ya motokaa, ndugu wa Wright wakaja na kuunda ndege, ingali ni nguvu za farasi (Mnaona?), mnaona, lakini imeboreshwa.

54 Moja huambatana na lingine. Tukio moja huambatana na tukio lingine wakati wote. Sasa, kama mambo. . . Sasa, msikose kupata hii. Fungueni masikio, moyo, na kila kitu sasa, na msikilize kwa makini.

55 Kitu chochote kinapotokea duniani, ni onyo kwetu kwamba kitu fulani kinakaribia kuwa. . . kutokea Mbinguni. Kile mwanadamu anachofanya duniani kwa mafanikio yake, ni kitu ambacho Mungu anajiandaa kufanya kwa ufanisi Wake kwa kanisa Lake. Sasa, tunaangalia, kwamba tulipotoka kwa farasi na mkokoteni, motokaa, ndege, kanisa, Mungu ameweza, katika ulingo wa kiroho, kufanikisha kutoka kwa kuhesabiwa haki kupitia Luther, utakaso kupitia Wesley, hadi kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu sasa. Mnaona? Ni mfano, kivuli, mafanikio, yale ambayo Mungu ameweza kufanya.

56 Sasa. Sasa, kumbukeni, Mungu kwa Luther kwa nguvu za Roho Mtakatifu, Aliweza kufanikisha kwa Luther kwa kanisa, kuhesabiwa haki. Basi kanisa lilipopata kuhesabiwa haki, kutoka katika kanuni za imani za Kirumi, lilianza kupata Uhai na kuanza kusonga mbele, kupitia kuhesabiwa haki. Mungu aliweza kufanya hivyo kupitia mafanikio Yake kumfanya mtu mmoja kusimama kimya muda mrefu vya kutosha ili aweze kujidhihirisha Mwenyewe kwa hilo, na kuwapelekea watu ujumbe Wake. Vema.

57 Mafanikio mengine Mungu aliweza kufanya, alimpata mtu, kwa, John Wesley, kusimama kimya vya kutosha, angeondoka kwenye kanuni za imani za Kilutheri, ilipokuwa imefikia, kuhubiri utakaso. Ndipo kanisa likatoka kwenye farasi na mkokoteni, hadi kwenye motokaa. Lilipata Uhai zaidi na kuanza kukimbia. Likaanza kwenda mbio zaidi kidogo basi.

58 Ndipo basi ukaja Mtaa wa Azusa, ambapo waliondoka ardhini wakaingia hewani kupitia ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mungu akaliondoa kanisa kutoka katika kanuni za imani

zilizobanwa ardhini na kulirusha hewani katika safari ya pekee. Wakati tu ndege ilipoingia, Roho Mtakatifu akaingia nyuma yake. Mnaona? Hiyo ni kweli.

59 Kuhesabiwa haki, farasi na mkokoteni; utakaso (Ulikuwa ni nini?), motokaa ikaanza kwenda mbele. Kisha ubatizo wa Roho Mtakatifu, ukaondoka ardhini, tukainua miguu yetu, tukaingia hewani, tukiruka kote mbinguni pamoja na karama za Kimbinguni, kunena kwa lugha, uponyaji wa Kiungu.

60 Hao, walikuwa bado katika motokaa, na bado wakiendesha farasi na mkokoteni, walifikiri hilo lilikuwa ndilo jambo la ajabu sana walilopata kuona, hao watu walikuwa na kifafa. Lakini waliondoa miguu yao ardhini. Mungu aliweza kuliletea kanisa mafanikio Yake, wakati alipopata kundi la watu wamesimama kimya muda mrefu vya kutosha hata angeweza kumimina Roho Wake ndani yao.

61 Nguvu zile zile za farasi zinazoweza kumdundisha farasi zilifanya vivyo hivyo kwa motokaa, na kufanya vivyo hivyo kwa ndege. Naye Roho Mtakatifu yeye yule aliyeliletea Kanisa kuhesabiwa haki, Yeye alileta mwingi zaidi wakati alipoleta utakaso, na kuumwaga ndani pamoja na Roho Mtakatifu, zingali ni nguvu zile zile. Kweli. Akaingiza kitu kile kile ndani, akaliondoa kanisa ardhini akalipeleka angani. Vema.

62 Sasa, mambo yamebadilika kabisa (Mnaona?), kwa sababu sayansi inasonga mbele. Na sikuzote tunazungumza kuhusu sayansi, lakini hebu tuangalie nyuma tuone kile Mwalimu wetu mkuu wa sayansi anafanya. Tuangalie kile Mungu anachofanya na kanisa Lake.

63 Sasa, tumeingia kwenye ule wakati, si wa—wa farasi na mkokoteni tena, sio motokaa tena, sisi. . . sio ndege tena, sasa, kuna wanaanga. Loo, jamani. Huu ni wakati wa mwanaanga. Loo, ni jambo kubwa jinsi gani.

64 Farasi na mkokoteni havingeweza kuondoka duniani bali sasa tuko katika wakati wa mwanaanga. Na kanisa vivyo hivyo. Hilo ndilo badiliko kubwa ambalo siwezi kulileta mbele za watu. Wametulia kwenye ndege. Baadhi yao wametulia kwenye farasi na mkokoteni. Lakini Mungu ana wakati wa mwanaanga.

65 Loo, ni wakati wa jinsi gani wa kuishi. Si ajabu hawawezi kuuelewa. Lakini, mnaona, Mungu anapomwacha mwanadamu kufanya jambo fulani, ni kulionyesha kanisa kwamba Yeye anafanya jambo fulani.

66 Mnaona, daima wanajaribu kurudisha kitu hicho cha kale. Na sasa, kuweka farasi na mkokoteni, ni ninii tu. . . ni mabaki, ni historia. Vilikuwa sawa katika siku zake, lakini siku hizo zimepita. Utukufu. Kupeana mikono na mhubiri kulikuwa ni sawa, zamani za kale, lakini huo umepita sasa. Madhehebu yalimaliza siku zake. Tumepita hapo sasa.

67 Tuko katika wakati wa mwanaanga. Amina. Sasa, ninaanza kujisikia kubarikiwa. Um-hum, uh-hum. Wakati wa mwanaanga, huo ndio umewafanya watu kupinduka kabisa. Hawajui wawazie nini juu ya mambo haya. Mnaona? Hawajui jinsi ya kuyapata. Angalieni. Hata hivyo, wakati huu wa mwanaanga ni Roho yeye yule, nguvu zile zile, kama tu nguvu za farasi zilivyokuwa.

68 Sasa, katika wakati huu wa mwanaanga katika mambo ya kawaida, pia kuna wakati wa mwanaanga katika kiroho. Ni kitu gani? Ndipo kanisa kutoka kwa ndege, kama ya asili, limechukua safari ya juu zaidi. Mbona, huyo mwanaanga, hakuna ndege itakayomshika. Amefikia mahali ambapo hawezi hata kuiona ndege tena. Mnaona?

69 Na hivyo ndivyo Mungu anavyofanya sasa. Badala ya maskini jamaa mdogo wa shule kujitokeza, na kuzungumza kuhusu mambo fulani ambayo Dk. *Nanii* alisema miaka iliyopita, tunao tai, manabii, wanaopaa hata mbinguni, mbali sana na wazo la kuku lililobaniwa duniani. Wakati wa mwanaanga. Mungu ameuthibitisha. Utazame.

Kama ilifanyika katika siku za farasi na mkokoteni, na siku za motokaa, katika Luther, Wesley, vipi kuhusu sasa? Kuna nini?

70 Watu wakizungumza juu ya kuwa wa kisasa, waliita huo wa kisasa. Huu ndio wa kisasa. Huu ndio wa kisasa, kulingana na Ufalme wa Mungu, wanaanga. Utukufu. Wakati wa mwanaanga, hakika, tai, manabii wa Mungu wakijitokeza jukwaani. Jinsi tunavyoshukuru sana kwa hilo.

71 Ni kitu gani? Madhihirisho ya kiroho ya Neno la kiroho yakitimizwa dhahiri mbele zetu. Amina. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

72 Neno la Mungu lililodhihirishwa, wakati mmoja lililokuwa gumu ku—kuelewa, sasa, linafanywa dhahiri kupitia mwanaanga. Mahali pa kanisa ambalo linapaswa kuwa moja kwa moja huko mbinguni, sio hapa chini likielea kote kupitia mawinguni, na kunguruma kama ndege, lakini kitu ambacho kinasukumwa mbele na kitu Fulani kinachoirusha mbele kupita kitu chochote ambacho ndege ingeweza kuwazia. Ni mwanaanga. Huo ndio wakati tunaoishi sasa, wanaanga wa kiroho.

73 Sasa, mwanaanga anaweza kuona vitu ambavyo farasi, mkokoteni, motokaa, au ndege hata hazingeweza kuona, kwa sababu yuko maelfu ya maili mbele yao. Yuko mbele sana mpaka wananinii. . .na mara hamsini spidi yao. Amina.

74 Sasa, unaona ni kwa nini watu wanafikiri unaingia kichaa? Hawawezi kulielewa. Mbona, bado anapanda mzee Farasi. Kwani Farasi ana spidi gani? Ni sawa, lakini Farasi ana spidi gani ukilinganisha na ya mwanaanga?

75 Vivyo hivyo kuhesabiwa haki kuna spidi gani ukilinganisha na ufunuo na Uwepo wa Yesu Kristo kukupeleka mbali sana na hapo, pa kujiunga na kanisa, ama kupeana mikono na mtu fulani. Ni wakati wa mwanaanga, ambapo kanisa linapaswa kuinuliwa juu, juu sana kupita kila kitu. Hiyo ni kweli.

76 Mwanaanga wa kiroho ni tai. Yeye huruka juu kupita kanuni zote za imani za kimadhehebu, vizuizi vyote vya kimadhehebu, mawazo yote ya kimadhehebu, mawazo yao yote yenye mawingu.

Yuko juu ya kila wingu, kila kitu kilichopo cha kutazama, yuko juu ndani ya . . . karibu na nyota: mwanaanga.

Naye mwanaanga mwaminio pia yuko juu mbinguni. Yeye yuko mbali sana na vitu hivi vilivyoshikamana na dunia. Yuko juu sana. Yuko kwenye anga za juu.

Mnaona, mtu wa duniani hajui mengi sana kuhusu anga za juu. Lakini ikiwa mwanaanga yuko kwenye anga za juu, yuko huko pamoja nayo.

77 Na hiyo ndiyo sababu kanisa siku hizi halielewi. "Kwa nini unanena kuhusu dhehebu? Kwa nini unakemea *hili*? Vipi kuhusu *hili* hapa, *hili* hapa? Sielewi upambanuzi huu. Sioni jinsi . . . ingeninii vipi . . . hiyo inawezekanaje?" Hakika. Wewe umefungwa ardhini. Kweli.

78 Unaona, wakati wa mwanaanga umeinuliwa juu ya hayo, huko juu yake kabisa, juu sana ya Mtaa wa Azusa, juu sana kuliko mengine yote. Ndilo jambo la kisasa zaidi tulilo nalo, ni mwanaanga. Amina. Mungu hatafuti wapanda farasi na mkokoteni. Anawatafuta wanaanga, mtu fulani anayeweza kuruka na kwenda kupita mahojiano.

Sasa, mtu fulani anasema, "Sasa, ngoja kidogo, ndugu. Je, si ni jambo la busara kwamba sisi . . . "

79 Hii ni zaidi ya hoja. Iko katika anga ya juu, nje ya mahali pa hoja. Tunapaswa kuzitupa chini. Kwa hiyo unapokwenda juu yazo zinatupwa chini, kwa sababu ziko chini yako. Anga za juu, mwanaanga, ameinuliwa juu ya mawazo yote ya binadamu. Uko katika Uwepo mtukufu wa Kristo, naye Kristo yu ndani yako.

80 Mwanaanga wa asili anadhibitiwa na kitengo cha rada ardhini. Rada hii inamdhibiti. Mmetazama hili labda kwenye televisheni. Wakati wanapopanda juu, jinsi maili na maili na maili usingeweza kuona kitu au chochote, na bado rada hii inaelekeza moja kwa moja kwake. Anadhibitiwa na rada, mwanaanga wa kawaida.

81 Na mwanaanga wa kiroho anadhibitiwa na kitengo fulani pia, kitengo cha maombi. Hayo humwogoza mwanaanga wa kiroho, yanamfanya alainike, uh-huh, ni maombi. Loo, ni vizuri, nawaambia.

82 Mungu alikuwa na kitengo kidogo kilichowekwa duniani wakati mmoja wakati Mwanaanga Wake wa kwanza alipokuwa

hapa. Nanyi mwajua, mguso mmoja mdogo wa imani ulimsimamisha, nao ukamjibu.

83 Maombi hubadilisha mambo. Hubadilisha nafasi kwa maombi ambayo yanaweza kudhibiti. Mnaona, tunaweza kuona kile kinachoweza kufanywa katika mambo ya kawaida, na ni mfano wa matukio ya kiroho. Kinaweza kudhibitiwa kwa njia hiyo.

84 Sasa, kwa kuwa sayansi imesonga mbele hadi angani hata inawabidi kumchukua mwanaanga, halafu, kanisa limesonga mbele, nanyi mnaona, kila wakati linapopungua, huhitaji kudhibitiwa na machache.

85 Sasa, tunaona ya kwamba ya kiroho na ya kimaumbile yanafanana. Kwa hivyo tunaona kwamba ya kimaumbile yameenda mbali sana, mpaka saa ya kimaumbile, inasema kuwa ni usiku wa manane kasoro dakika tatu. Wazieni hilo. Sayansi inadai kwamba zimebaki dakika tatu ifike usiku wa manane. Jambo fulani liko karibu kutukia. Wanaweza kulihisi. Na kama wangeweza kulihisi, ni zaidi sana vipi kanisa linapaswa kuwa na uwezo wa kulihisi? Ikiwa wanaweza kuona jambo fulani linaenda kutukia, ni zaidi sana vipi sisi tunapaswa kuona jambo fulani linaenda kutukia?

86 Sasa, lakini wanasema, kwenye saa yao, ni dakika tatu kufikia saa sifuri kwa jambo fulani kutukia. Kwa hiyo mnajua walifanya nini? Waliogopa, kisha wakaingia kwenye bomba lao la mwanaanga, nao wanahesabu kinyumenyume. Nao wataiacha dunia hii. Wanaelekea mwezini. Kila mtu anajaribu kufika mwezini, wanataka kuondoka duniani kwenda mwezini.

87 Hivi hamwoni matumizi ya kiroho? Mwanaanga wa kiroho aliingia ndani ya Yesu, akisikiliza kuhesabu kinyumenyume kwa Neno la Mungu, na anajiandaa kuondoka kwenda Mbinguni. Hiyo ndiyo tofauti. Loo, jamani. Hilo linasikika lisilo adilifu, lakini ni ukweli. Hebu angalieni tu nyuma kupitia historia. Angalieni nyuma kupitia wakati muone kwamba kila kitu. . . chochote cha kimaumbile kilichotokea duniani, Mungu alikifanya kitendeke kiroho, akiliinua juu kanisa Lake. Hili hapa, papa hapa mbele zetu, na hiyo ni kweli. Tunalijua, tunalielewa.

88 Mungu ana mfumo mpya. Sio ule mfumo wa kale; ni mfumo mpya. Yeye analiinua Kanisa Lake juu. Wanazidi kupungua katika uchache wakati wote. Walipungua katika siku za Nuhu, walipungua katika siku za Lutu. Daima hupungua, mpaka wanakuwa wachache sana, sana. Lakini bado hiyo Punje ndogo ya Mungu ingali inasonga mbele, ikiendelea kupata nguvu zaidi, na zaidi, wakati wote.

89 Kanisa la kweli la Mungu aliye hai liko maili nyingi sana mbele barabarani kuliko lilivyokuwa. Tunaliona. Tunalijua. Ni kweli.

90 Simaanishi shirika. Sasa, mmerudi chini kwenye farasi na mkokoteni tena. Mnaona? Tunapanda juu kuliko kitu hicho. Hatutaki kukirudia kitu hicho tena. Hapana, inanipasa kusema la. Vema.

91 Mwanaanga wa kiroho yuko ndani ya Kristo, naye anasikiliza Neno la Mungu, kule kuhesabu kinyumenyume, kuona linaelekea wapi. Naye anajitayarisha kuondoka sasa, sio kwenda mwezini, ataupita mwezi upesi sana. Anaenda zake Mbinguni, na anasikiliza kule kuhesabu kinyumenyume. Naam, anaelekea Mbinguni katika Unyakuo, wa utukufu wa Mungu. Yuko ndani ya Kristo, amevikwa utukufu Wake, akielekea Mbinguni pamoja Naye, anaondoka duniani.

92 Watu wa kawaida walisimama wameduwaa, mnakumbuka, miezi michache iliyopita, wakati John Glenn alipoingia kwenye bomba hilo kuwa mwanaanga. Nao wakasimama wameduwaa, taifa liliduwaa, walipoanza kuhesabu kinyumenyume. Wakaanza, "Kumi, tisa, nane, saba, tano, sita, nne, tatu, mbili, moja, sufuri."

93 Ndipo huyo mwanaanga mkubwa alipoanza kuachilia nguvu za atomiki ndani yake, moto ukaanza kuruka nao wakaondoka, ulimwengu mzima ukasimama umeshtuka. Bila shaka. Angalieni.

94 Lakini mliona? Kila mara, hesabu yao ya kinyumenyume ilikuwa ni ya kurudi nyuma: "Kumi, tisa, nane, saba, tano, sita, nne, tatu, mbili, moja, sufuri." Hivyo ndivyo ulimwengu unavyofanya sikuzote, kwa vyovyote vile, ulikuwa ni kinyumenyume. Ndivyo ulimwengu unavyofanya chochote. Hivyo ndivyo mwanadamu anavyofanya. Ni kurudi nyuma kutoka kwa Mungu. Mnaona?

95 Na kwa vyovyote vile, kumi si nambari ya kiroho katika Biblia. Mtu yeyote anajua hilo. Namba ya Mungu ni saba. Hiyo ndiyo namba Yake kamili. Naye Mungu, nambari Ya—Yake kamili ni saba. Naye Mungu, kuhesabu Kwake kinyumenyume huanzia moja. Kweli. Mwanadamu anaanza na kumi, anarudi nyuma. Mungu huanzia moja, na kuenda mbele.

96 Mwanadamu alianza hesabu yake, kuhesabu kwake kinyumenyume, naye Mungu akaanza hesabu Yake ya kwanza. Mngependa kujua wakati alipoanza? Alianza katika A.D. 33, hapo alipoanza kuhesabu nyakati Zake saba za makanisa. Alipozimaliza, ilikuwa ni sawa. Kweli. Hivi ndivyo Mungu alivyohesabu kutoka moja hadi saba: "Efeso, Smirna, Pergamo, Thiatira, Sardi, Filadelfia, Laodikia, sufuri." Amina. Kweli. Mnaona, sufuri inakuja baada ya Laodikia. Tumeshaupita wakati huo sasa. Limekuwa vuguvugu nalo likatapikwa, mambo yake yote yakaanguka.

Lakini tuko ndani ya Kristo, na Kristo amehesabu nyakati za kanisa Lake. Kuna saba tu za hizo. Ni Biblia.

97 Ndio kwanza tuzipitie Ma—Maskanini, tukionyesha kila mmoja: nyota zao, wahudumu wao, na Nuru ya siku hiyo; na kushuka hadi kwa Luther. . . ; na wa Filadelfia, John Wesley; na kuendelea hadi Laodikia; kila wakati; jinsi kuanguka kungekuja; na kile *huu* ungekuwa; na yale Maandiko yalisema wangefanya; na hayo hapo. Tumeyapata katika historia, sawa hasa.

98 Na sasa tunapita wakati wa Laodikia. Sote tunajua hilo. Kila mmoja wetu anayeijua Biblia anajua hiyo ni kweli. Vema, hesabu iko wapi basi? Ni saba. Na inayofuata ni sufuri. Mnaona? Ati nini? Efeso ulikuwa wakati wa kwanza wa kanisa; Smirna, wa pili; Pergamo, wa tatu; Thiatira, wa nne; Sardi, wa tano; Filadelfia, wa sita; na Laodikia, wa saba.

99 Sasa, tulipitia katika wakati huo wa Kipentekoste; tumepitia wakati wa Kilutheri; tumepitia wakati wa Wesley. Basi angalieni. Mara kanisa lilipoanza, Mungu alianza kuonyesha ishara duniani, akionyesha kwamba alikuwa akiliendeleza kanisa Lake kutoka katika kuhesabiwa haki, hadi utakaso, hata kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu, sasa kufikia mwanaanga. Amina. Hicho ndicho tunachotafuta, ni wanaanga, mtu anayeweza kujiepusha na kitu hiki hapa kisichoweza kujiondosha duniani: inabidi awe mfuasi wa shirika fulani, ama kitu kama hicho.

100 Mungu anamtafuta mtu ambaye anaweza kupanda juu sana kama tai, aruke, na aende moja kwa moja mbinguni huko ng'ambo, ambako mambo yote yanawezekana juu kuliko mlio huu wa kuku wa humu duniani: akiendesha kwa silinda nne; na kidhibiti joto kikapasukia ndani, hata hawajui jinsi ya kubatizwa bado (Loo, jamani!); na kuzozana huko kote na kupiga makelele. Tunaruka mbali nayo. Amina. Mbona, naam.

101 Nafikiri hivi, marafiki: Kama taifa zima lilisimama kwa hofu, na kutazama kupitia kwa televisheni wakati kuhesabu kinyumenyume kulipofika kwa mwanaanga huyo, John Lynn, uh, Glenn, kuondoka akielekea kwenye safari yake ya kwanza kuelekea mwezini, akainuka juu ya hayo, nayo dunia nzima ikasimama kwa mshangao walipomwona yule mwanaanga akiondoka; ulimwengu wote utasimamaje wakati yule Tai mkuu wa Kanisa la Mungu, wakati atakapoyatandaza mabawa Yake makubwa moja ya asubuhi hizi, akisukumwa na Roho Mtakatifu na Moto, atakapoanza mtetemo Wake kutoka ardhini na kwenda mbinguni? Ulimwengu wote utajua. Malaika watawakaribisha ndani kwa shangwe. Amina.

102 Tunaishi katika wakati wa mwanaanga, tukielekea mbinguni. Watu hawawezi kulielewa. Vema, nena juu ya mshtuko unaokuja, ngoja tu hadi Kanisa hilo litakapoanza kwenda juu, wakati yule Tai mkuu anayeitwa Kanisa la Mungu, lililokombolewa kwa Damu ya Yesu Kristo, atakapozitandaza

mbawa Zake, nazo nguvu za Roho Mtakatifu zitaanza kuliinua kutoka ardhini. Utakuwa ni wakati mzuri sana.

103 Kumbukeni, motokaa haiwezi kulifuata; wala ndege. Ni mwanaanga. Hebu tuwe mwanaanga. Hebu tumwamini Mungu. Sasa, wewe ninii tu, unaona ni nini.

104 Sisi ni . . . sote tunapenda kuzungumza kuhusu ule Mtaa wa Azusa. Tunapenda kuzungumza juu ya miaka hamsini iliyopita. Na nimewakemea juma zima, nikiwaambia juu ya mahali ambapo sisi . . . tumepoteza umbali gani kutoka hapo. Lakini tumepiga hatua sana katika Roho wa Mungu katika mambo mengine, tuliyo nayo sasa, ambayo hata hawakuwahi kuwa nayo huko nyuma.

105 Walikuwa ndio kwanza waache motokaa, wakainua miguu yao hewani, kusudi waweze kupata karama chache za kiroho, kunena kwa lugha, na kupaza sauti na kuimba nyimbo za kiroho. Mbona, walikuwa wakielea huko juu kama vipepeo. Mnaona? Bila shaka. Huo ulikuwa wakati mkuu.

106 Lakini, loo, ndugu, tumeinuliwa mbali zaidi ya hapo sasa. Kanisa liko mbali sana na hapo, Kanisa la kiroho. Liko katika wakati wa tai sasa, mwanaanga, likiendelea kuruka juu, na kuangalia chini kwa kuku raia mwenzake. Mnaona? Tuko juu mbali sana na hapo, huko juu kabisa mbi—mbinguni, ambapo Kristo anakuwa ni Kitu kamili kinachochukua mamlaka kabisa, na kuishi Maisha Yake, na kutenda kupitia kwako, sawasawa na alivyofanya hapa duniani.

107 Wakati wa mwanaanga, kuhesabu kinyumenyume kunaendelea, ndugu. Ninaamini kanisa ni . . . mshiriki wa mwisho atazaliwa ndani yake, labda usiku wa leo. Yule wa mwisho ataingia.

Sasa, angalieni, najua huu umevunjika-vunjika, nao muda wangu unakwisha, lakini tazameni. Sitaenda mbele zaidi, lakini angalieni hili.

108 Mnaona kwamba maendeleo ya Kanisa yamefuata maendeleo ya wakati. Mnajua hilo. Na tumebadilika sasa kutoka kwa ndege hadi mwanaanga. Na lazima kuwe na mabadiliko. Nasi tumeona mabadiliko matatu yaliyotokea katika maendeleo ya usafirishaji, ya nguvu, na kila mara huchukua nguvu za kuongezewa, nguvu zilizoongezewa, nguvu zilizoongezwa, kuweka zaidi, na zaidi, na zaidi.

Kwa nini ndege isifike huko juu? Haina uwezo wa kufanya hivyo. Haijajengwa kwa ajili hiyo. Isingeweza kufanya hivyo.

109 Mwanaanga ana nguvu. Bomba ambalo yuko ndani yake, lina nguvu. Yuko huko juu. Anapanda juu. Anarushwa juu kama kwa elektroniki, kwa—kwa atomi, ambayo ni nguvu kubwa zaidi kuliko petroli au kitu chochote ambacho tumewahi kuwa nacho hapo awali. Mnaona? Tuko katika wakati mwingine.

110 Na shida yake ni, kwamba sayansi inaendelea kusonga mbele katika mafanikio yao, lakini kanisa linataka kutulia na kubaki likipanda maskini Farasi mzee mtaani. Naam, bwana. Hiyo ni kweli. Unashuka chini, "Mama yangu alijiunga miaka mingi iliyopita, unapaswa kujiunga pia." Unaona? Usifikirie juu ya jambo kama hilo. Hebu tuinuke. Mambo yote yanawezekana.

111 Sayansi ina mti wanaoweza kupanda. Lakini wanaweza tu kupanda hadi umbali fulani, halafu wao. . .huo ndio umbali wanaoweza kwenda. Huo ndio mwisho wa utafiti wa kisayansi. Wanajiua wenyewe.

112 Lakini mnaona, kwenye Mti wa imani hakuna mwisho wake. Unaendelea tu kwenda. Huo ndio Mti tunaopaswa kuwa juu yake usiku wa leo, Mti wa Uzima, Mti wa imani. Si kuelekea mwezini, ni kuelekea Mbinguni, kuelekea kwa Mungu, pamoja na unyakuo wenye utukufu wa Bwana Yesu katika Uwepo Wake, na nguvu Zake, na Uhai Wake wenyewe kutoka Mbinguni. Sio kushuka na kutufanya tujiunge na kanisa, si kushuka hata kutufanya tupaze sauti, bali kushuka kuuacha Uhai Wake wote uishi kupitia kwetu.

113 Kuishi katika mbingu, kujipeleka mbali, hata utakapoona mambo yajayo, yaliyokuwako, na yatakayokuja; kuinuka juu ya kitu chochote ambacho kanisa limekuwa nacho tangu siku ambazo Kristo alikuwa duniani. Na tunazifurahia leo. Hakika. Tuko katika wakati mkuu, rafiki, wakati mzuri sana, wakati wa mwanaanga.

114 Mungu, tupe wanaanga, tupe wanaume na wanawake, wanaume hodari, wanawake hodari. John Glenn na hao wengine walipaswa kufanya nini walipoingia kwenye bomba hilo? Walikuwa ndio waanzilishi. Mungu anataka waanzilishi wa Neno hili, wanaanga ambao watachukua vitu tulivyo navyo, na kuwa, sio kuridhika navyo, lakini tunaendelea mbele. Mungu anapata mafanikio.

115 Sasa, ati nini? Itachukua imani ya mwanaanga kukusafirisha kutoka dunia hii ili kukutana na Yesu. Hiyo ni kweli. Usipotaka kuachwa bikira aliyelala, basi afadhali uingie kwa mwanaanga sasa hivi, na upande juu ya mambo haya. Uko juu na umeruka juu yake.

116 Ni vigumu kwa watu kuelewa hilo. Hawajawahi kuliona. Ni kitu kipya. Lakini ni vile vile, imethibitishwa ya kwamba ni ninii ya Mungu. . .Moja ya mafanikio Yake ya mwisho na ya hivi punde zaidi ni kujidhihirisha Mwenyewe na kusema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya."

117 Si ajabu walipompata yule Mwanaanga wa kwanza duniani, Kristo, akiwa Mungu aliyedhihirishwa, wakati yule mwanamke alipogusa vazi Lake, aliponywa. Wakati Petro alipokuja Mbele Za—Zake Naye akasema, "Jina lako ni Simoni. Wewe ni mwana wa Yona," hao wanatheolojia, jamaa hao wa farasi na mkokoteni

hawakujua tu jinsi ya kuelewa jambo hilo. Huh? Wasingeweza. Wao. . . Wala hawawezi siku hizi. Hawawezi kuelewa.

118 Nasi tunaona ya kwamba wakati aliposimama pale, na yule mwanamke kisimani, Alimwambia dhambi zake, na kile alichokuwa amefanya. Naye akaingia, akawaambia watu mjini, "Njoni, mwone Mtu Ambaye aliniambia mambo ambayo nimefanya." Mbona, hilo lilikuwa ni jambo la kushangaza jinsi gani. Walijua ilibidi iwe ni kitu tofauti na walichokuwa nacho.

119 Si ajabu Nikodemo, yule mwanachuoni mkuu, alimjia Yesu na kusema, "Rabi, tunajua Wewe ni mwalimu uliyetoka kwa Mungu, kwa maana hakuna mtu awezaye kufanya mambo haya isipokuwa Mungu awe ndani yake."

Ndipo Mwanaanga huyo huyo akasema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya."

120 Tuko tayari kuruka. Kuhesabu kinyumenyume kunaendelea. Je, mko ndani? Tunahesabu nini? Efeso; Smirna—Smirna; Pergamo; Thiatira; Sardi, Lutheri; Filadelfia, Wesley; Laodikia, Pentekoste. Tumeupitia sasa. Ni upi unaofuata? Saba tu. Huna nane.

121 Loo, ninawezaje kunyamaza ninapoona mambo haya? Ninawezaje kusimama kimya, Ndugu Lyle? Ninaweza kufanya nini ila kufanya kile ninachofanya? Hakuna wakati mwingine ujao. Ni wanafunzi wangapi wa Biblia hapa ndani wanaojua hiyo ni kweli? Inueni mikono yenu, watu ambao. . . si wakati mwingine. Basi ni nini kinachofuata? Sufuri, unyakuo. Kwa nini ninataka jengo la dola milioni moja? Um-hum.

Hema au nyumba ndogo, kwa nini nijali?
Wananijengea jumba la kifalme kule!
Ya mayakuti na almasi, na fedha na dhahabu,
Hifadhi zake zimejaa, ana mali isiyosemeka.

Mimi ni mwana wa Mfalme!

122 Loo, sitaki hazina za dunia hii. Nina hazina Mbinguni. Asante Mungu. Siku moja niliingia kwenye bomba la Mwanaanga, Mwili wa Yesu Kristo, nikabatizwa mle ndani na Roho Mtakatifu, na kuangalia, kusubiri, kusikiliza kuhesabu kinyumenyume. Niliona nyakati zikija, zikija, zikija, zikija, mpaka wakati wa mwisho ukahesabiwa na kupita. Pumzi inayofuata. . . Ni zaidi ya dakika tatu, namaanisha, *chini* ya dakika tatu, sayansi inasema ni dakika tatu kwa dunia kulipuliwa, kwa wakati, ni chini ya hapo. Pumzi inayofuata ya Yehova ni, "Tokeni kwake, enyi watu Wangu. Njoni huku juu." Amina.

123 Tunaangalia papa hapa kabla wakati huo haujaja, na kuona nguvu tukufu za Mungu zikirudi kwa Kanisa; Uwepo wa Yesu Kristo, uwepo ulio kila mahali, akionyesha kile alicho, na pale Yeye alipo, na moja kwa moja miongoni mwetu akifanya kazi

zile zile alizoahidi zingefanywa katika wakati huu. Huyu hapa, akithibitisha ya kwamba Yeye ni yule yule.

124 Waebrania 13 inasema, "Yesu Kristo . . . " 13:8 ilisema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Naye huyo hapo katika wakati Wake wa kuhesabiwa haki kwa Luther. Kulikuwako na Kristo katika wakati Wake wa kutakaswa kwa Wesley. Kulikuwako na wakati Wake katika Mtaa wa Azusa, Wapentekoste, Walaodikia. Kwa ajili ya nini? Ilikuwa ni nini? Wakati wa ndege, Kipentekoste. Sasa huyu hapa katika mwanaanga, anayeishi ng'ambo, anayeenda kwenye anga za juu.

125 Ndege isingeweza kamwe kufika kwenye anga za juu, lakini mwanaanga anafika. Utukufu kwa Mungu. Ninasikiliza kuhesabu kinyumenyume. Loo, jamani. Kwa nini tunasubiri? Saa sufuri, saa ambayo Yeye . . . inapiga. Tumepita wakati wa Kipentekoste. Waliuundia madhehebu, na wakatoka kule wakizozana, wakarudi moja kwa moja katika Babeli kama hao wengine. Nao wana nini siku hizi?

126 Sikilizeni. Ni lini angewatapika tu? Walipopata uvuguvugu. Na ni wakati wa kutapika. Anawakataa. Ndipo basi anawachukua masalia kutoka kwake, nako kuhesabu kinyumenyume kumekwisha, naye Mwanaanga ameelekea Mbinguni.

127 Hima twende, ndugu. Hima twende, dada. Kuwa na hakika. Usi—usibahatishe. Usitegemee tu ujuzi fulani wa Kilutheri, au ujuzi wa Kimethodisti, au ujuzi wa Kipentekoste. Na tupande juu mbinguni sasa, tuingie juu katika haki ya Mungu, juu katika uweza Wake, juu kuona ya kwamba Kristo anaweza kuja ndani yako, na kujidhihirisha Mwenyewe sawasawa na alivyofanya alipokuwa hapa duniani. Mnaamini hilo? Ninaamini ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

128 Ni saa tatu kasoro dakika tano, ama saa tatu kasoro dakika saba. Huo ni wakati mzuri wa kumalizia. Mara saba, dakika saba zaidi. Ikiwa utaunyenyekeza moyo wako dakika saba zaidi, Yesu Kristo atathibitisha ya kwamba yuko papa hapa jengoni usiku wa leo. Um-hum. Hmm. Amina.

Ni vigumu kwa madereva wa farasi na mkokoteni kuona hilo, lakini lipo hata hivyo. Amethibitisha. Tuko kwenye wakati wa mwisho. Yuko hapa.

129 Ameahidi, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Siku hiyo, kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena. Hata hivyo ninyi mtaniona, kwa maana Mimi, Mimi nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu," hapa mwishoni mwa wakati. Na sisi hapa. "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu. Siku hiyo mtajua ya kuwa Mimi ni ndani ya Baba, Baba ndani Yangu, Mimi ndani yenu na ninyi ndani Yangu." Huyo ni Mungu katika watu Wake, Mungu kabisa.

130 Je, Mungu angetendaje akiingia katika mwili wa mwanadamu? Mwangalie Yeye. . . kile Yeye alichokuwa wakati alipokuwa katika mwili wa binadamu. Ati nini? Je, alijivunia kuwa hivyo? Hapana, bwana. Yeye alisema, "Sifanyi lolote mpaka nimwone Baba Yangu akinionyesha kwanza." Angalia jinsi alivyojithibitisha Mwenyewe, jinsi alivyokuwa thibitisho la kuwa Masihi. Alikuwa nabii. Alijua. Angeweza kuwaambia watu. Aliyatambua mawazo yao. Anaujua moyo wako. Anajua yote kukuhusu, anajua yale umefanya. Anajua unachohitaji. Anaweza kuzungumza nawe kupitia dhamiri yako, kukwambia, kujaribu kukuonyesha hilo.

131 Ibilisi anaketi kwenye hilo bega jingine, kasema, "Angalia upande mwingine." Inategemea unataka kuangalia upande gani sasa. Ni hayo tu. Kama walivyosema kwenye uchaguzi, "Mungu alikupigia kura, ibilisi akapiga kura dhidi yako. Sasa, mahali unapopigia kura yako ndipo pataamua mahali unapoelekea." Hiyo ni kweli. Huna budi kumchukua Kristo. Huna budi kuchukua Neno Lake. Huna budi kumwamini.

132 Na kama Yeye. . . Kama Biblia ilisema ya kwamba alikuwa yeye yule jana, leo, na hata milele, basi hana budi kuwa yeye yule. Kweli kabisa. Sasa,. . . Je, unaamini hilo? Inua mkono wako. Ni wangapi wangetaka kuwa mwanaanga wa Mungu ambaye angeweza kusema, "Ninaweza kuliondokea shirika na kumwamini Kristo"?

133 Sasa, kama Kristo ni Kristo. . . Kama ningewaambia ya kwamba kulikuwa na roho ya John Dillinger ndani yangu, ni—ningekuwa na bunduki. Maisha ya kitu chochote yatajizaa yenyewe. Kilicho ndani kitajisukuma nje. Hivyo ndivyo kanisa lilivyo tupu. Mnaona? Jinsi watu wanavyofanya na kutenda, wanajiita Wakristo, inaonyesha tu utupu. Kristo anapokuwa mle ndani, Yeye hutenda kazi. Anasema.

134 Wahubiri wanasimama mimbarani, na kuogopa kusema mema na mabaya, wanahofu kusanyiko litawafukuza. Vipi kuhusu Kristo? Atakuondoa usiposema. Kwa hiyo wewe ni rafiki wa nani? Ni nani ambaye wewe. . .? Unataka kuwa rafiki wa nani? Una chaguo la kufanya. Kila mmoja wetu anapaswa kufanya chaguo hili. Mungu atusaidie tufanye chaguo sahihi. Yesu Kristo ndiye chaguo langu. Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

135 Baba wa Mbinguni, hapa leso zimewekwa juu ya dawati hili usiku wa leo. Hiyo inamaanisha kwamba kuna watu wagonjwa. Katika Biblia walichukua kutoka katika mwili wa Mtakatifu Paulo leso na nguo, wakaziweka juu ya wagonjwa, wakapona. Sasa, tunajua ya kwamba sisi si Mtakatifu Paulo, lakini Wewe ungali ni Yesu. Haikuwa ni yeye hapo mwanzo; ilikuwa ni Kristo. Nawe ni Mungu yeye yule unayefanya kazi kupitia chombo kile kile cha mwanadamu kama ulivyokuwa wakati huo. Jalia

Roho Wako, Bwana, alithibitishe Neno Lako, na kulileta sasa, na kuwaponya watu wanaowekewa leso hizi. Tunaomba hayo, katika Jina la Yesu.

136 Pia, Baba, kuna wale hapa usiku wa leo, labda, wanaotaka kufanya ma—wanaotaka kufanya mabadiliko, ambao wanataka kutoka kwenye kanuni zao za imani na kuingia ndani ya Kristo, Mwanaanga wa kweli, wa pekee anayeweza kutuchukua. Yeye Ndiye pekee. Hakuna mtu aliyepaa juu ila Yeye aliyeshuka, yaani Mwana wa Adamu. Baba, ni wakati tu tunapokuwa ndani Yake kwa ubatizo wa kiroho, tumejisalimisha kikamilifu katika Neno Lake, ndipo Yeye anapoweza kuishi kupitia kwetu, na kutenda, na kuonyesha Neno Lake . . .

137 Hawezi kubadilika kwa sababu Yeye ni Mungu. Uamuzi Wake wa kwanza ni mkamilifu. Hawezi kuubadilisha. Sisi ni—sisi tuna kikomo. Tunafanya makosa ya kila namna. Yeye hana kikomo na ni mkamilifu. Uamuzi Wake wa kwanza ni uamuzi mkamilifu, na hauna budi kubaki vile vile, nasi tunajua hilo, Baba.

138 Sasa, Yeye alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya." Hawezi kubadilisha uamuzi huo. Yeye alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Kama Uhai wa Kristo ukiwa ndani yako, kama nia ya Kristo, basi tunahusika na kufanya mambo ya Kristo. Alisema ishara hizi alizofanya zitafuatana na kila mwaminio anayemwamini.

139 Sasa, na ijulikane usiku wa leo, Bwana, ya kwamba Wewe uko katikati yetu. Sisi ni watu wanaopatikana na mauti, wanadamu. Mioyo yetu inawaka. Tunaona me—mema na mabaya. Tunaona kuinuka kwa sayansi. Tunaona kuinuka kwa kanisa. Tunaona nguvu za Injili, kile inachofanya. Nasi tunatambua hakuna wakati mwingine wa kanisa utakaokuja, uliotabiriwa katika Neno. Ulisema hakuna kinachoweza kuongezwa Kwake wala kuondolewa Kwake.

140 Ndipo tunaona ya kwamba sayansi inayo, mitambo yao mikubwa sasa, ambayo itawabeba kutoka ardhini. Baba, tumeliona likiainishwa kote katika wakati. Sasa, tunajua tuko kwenye mwisho. Jalia Kristo, Mwokozi wetu, atende kazi miongoni mwa watu Wake usiku wa leo na kutoa thibitisho ya kwamba Yeye yuko hapa.

141 Alisema, "Popote walipo wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, nitakuwa katikati yao. Watakapopatana katika jambo lolote, na wakaomba, watapewa."

142 Baba, jalia kanisa hili likugeukie Wewe kabisa. Naomba niweze, usiku wa leo, kujisalimisha *hivyo* Kwako, ili upate kujithibitisha Mwenyewe kwamba upo. Jalia washiriki wa Mwili Wako hapa ndani waweze kujisalimisha Kwako, ili sote tuweze kuuona utukufu wa Kristo wetu mkuu ukitenda kazi kati yetu, ukitupa hakikisho, Bwana, ya kwamba tumetoka katika wakati

wa kanuni za imani, kwamba tuko katika wakati wa mwanaanga wa neema ya Mungu. Tujalie, Bwana. Tunaomba katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

143 Ni wangapi wanaotaka kuwa mwanaanga kwa ajili ya Mungu? Um-hum. Mungu, tujalie. Sasa, Biblia ilisema kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. (Ninajitayarisha kuita mstari wa maombi.) Mnaamini hilo? Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

144 Sasa, kama Yeye yuko ndani yetu, Yeye ndani yenu, ndani yangu, basi ataishi kupitia kwetu, afanye kazi kupitia kwetu, ahubiri kupitia kwetu, afanye kazi kupitia kwetu, afanye kupitia kwetu, kwa maana si sisi, "Si ninyi mnaonena, bali Baba akaaye ndani yenu ndiye atakayenena." Kama tu vile asemavyo, "Si Mimi nizifanyaye kazi hizo, ni Baba Yangu akaaye ndani Yangu azifanyaye hizo kazi." Nyote mnaamini hilo.

145 Sasa, kuna wagonjwa wangapi humu jengoni? Inua mkono wako, useme, "Mimi ni mgonjwa. Nahitaji uponyaji." Popote pale tu, kote jengoni, au haja . . . vema, ni karibu kila mahali.

146 Sasa kumbukeni, tangu wakati huu na kuendelea, siwajibiki kwa mkosoaji, ama chochote kitakachotukia. Kwa hiyo kama huamini, huu ndio wakati wako wa kuondoka, unaona, kwa maana kumbuka, hawa hutoka kwa mmoja wakamwingia mwingine. Ni mara ngapi tumeona hilo? Mmoja kwa mwingine. Nimewaona wakianguka kwa kifafa, wakishikwa na kansa, wakafa, wakapoozea vitini mwao. Mnajua hilo. Ni wangapi wanaojua jambo hilo na walijua kulihusu? Na tazameni, iko kila mahali kwenye . . . vema, kila mahali. Kwa hivyo ni wakati wako wa kuondoka, endapo wewe ni mkosoaji. Usiketi hapa sasa, maana hakika utakuwa hatarini.

147 Waaminio, bakini vitini mwenu. Iweni wanyenyekevu. Hakuna watu wengi katika jengo hili niwajuao. Najua kanisa langu. Kuna baadhi ya watu kutoka kanisani kwangu. Dada Lyle, Ndugu Moore alikuwa hapa. Ni wangapi humu ndani wa—wanaojua kwamba sijui lolote kukuhusu wewe? Inua mkono wako. Huko, mnaona, ni karibu kila mtu.

148 Sasa, kama Kristo alikuwa amesimama hapa, nawe ulikuwa mgonjwa, vipi . . .? Unge—ungemwomba uponyaji? Hakika ungemwomba. Je, angeweza kukuponya? Angekwambia alikuwa tayari amekuponya. Kwa kupigwa Kwake uliponywa.

149 Lakini kwa ishara Yake ya Kimasihi kuonyesha ya kwamba Yeye alikuwa vile Musa alivyosema, na yale Mungu aliyosema: "Akiwapo mmoja kati yenu ambaye ni wa kiroho au nabii, Mimi, Bwana, nitajifunua kwake. Na ikiwa yale asemayo ni kweli, basi msikieni. Ikiwa sivyo, msiyasikize. Nitasema naye katika maono. Asemacho kikitimia, basi huo ni ukweli. Lakini kisipotimia, basi msikiamini."

150 Sasa, ninabashiri, na kuwaambia, ya kwamba Kristo yupo hapa. Ulimwengu wa kisayansi umethibitisha hilo kwenye picha. Na tuko karibu sasa.

151 Sasa, wewe uliye na shida, nataka uwe mnyenyekevu kadiri uwezavyo kuwa, nanyi muinamishe tu vichwa vyenu kwa muda kidogo, na muombe nyote pamoja. Na muamini tu sasa kwa moyo wenu wote kwamba Kristo yupo.

152 Iweni tu na imani. Msitie shaka, kila mahali huku. Iweni katika maombi. Ombeni tu kwa unyenyekevu, mseme, "Bwana Yesu, unirehemu. Ninajaribu kuamini." Tunaketi tukiwasiliana na Kristo, Mungu atusaidie. Mungu, utuhurumie kwa kutukaribia, wakati sisi tukiwaza kama wale wanafunzi walivyowazia, na kuongea, "Alipokuwa akiwaza juu ya mambo haya, tazama, Malaika wa Bwana akamtokea," Maandiko yanasema.

153 Iweni na kicho tu mioyoni mwenu, mkitazama, mkiamini. Sasa, mnapoinua vichwa vyenu baada ya maombi, sasa angalieni huku. Nanyi muamini sasa ya kwamba Kristo yu hai. Ungameni makosa yenu yote na kuamini kwamba Kristo yu hai.

154 Na sasa, ikiwa Yeye ni Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, basi akiwa ni yule yule jana, leo, na hata milele, angetendaje kama angeguswa? Mwanamke aliyeligusa vazi Lake, Yeye hakukuhisi kimwili, maana Yeye... vazi la Kipalestina linapwaya pamoja na vazi la ndani. Ndipo Petro akamkemea, akasema, "Kila mtu anagusa."

155 Akasema, "Naam, lakini ulikuwa mguso tofauti. Uweza, nguvu, zilinitoka." Naye akawaangalia kusanyiko Lake mpaka akamwona maskini mwanamke mmoja, naye akamwambia alikuwa akitokwa na damu, na imani yake ilikuwa imemwokoa. Sasa, hivyo ndivyo Kuhani Mkuu alivyotenda jana. Na kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, atatenda vivyo hivyo leo hii.

156 Sasa, kwa kuwa Yeye hana mwili wa kawaida duniani ila Bibi-arusi Wake tu, Yeye hufanya kazi kupitia huyo: mwanadamu. Yeye ni hivyo sikuzote, ilikuwa ni Mungu katika Eliya, Mungu katika Daudi, Mungu katika Kristo, sikuzote, mnaona, Yeye anao Mwili Wake duniani.

157 Sasa, haijalishi angenipaka mafuta kiasi gani, hana budi kukupaka mafuta pia. Mengi Yes-...mambo Yesu asingeweza kufanya Mwenyewe kwa sababu ya kutokuamini kwao. Tunajua hilo. Mnaona? Walisema, "Alifanya hivi huko Kapernaumu. Hebu tumwone akifanya hivyo hapa." Naye akastaajabu, akaenda zake, na kuwaacha, mnaona, kwa kutokuamini kwao.

158 Sasa, mwamini Yeye. Na kama ungeweza kuona kuonekana Kwake dhahiri, si ingekusaidia? Bila shaka. Vema, sasa, Yeye hawezi kuonekana katika mwili wa kawaida. Akionekana, wanaanga tayari wameondoka. Unaona? Ataonekana,

atakapokuja, kanisa limeondoka, mnaona, tunajua jambo hilo, ungeweza kuona ono Lake.

159 Lakini Uhai Wake uko hapa ndani. Sasa, kama kungekuwa na mtu amesimama hapa mwenye makovu ya misumari mikononi mwake, na alama za miiba, mnafiki yeyote angeweza kufanya hivyo. Naam. Lakini ungeamua kulingana na maisha yake.

Angalia kile Yeye . . . Hao, Wayahudi walimwambia, kasema, "Mbona, wewe ni mwanadamu ukijifanya mwenyewe Mungu."

160 Akasema, "Kama sizifanyi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Lakini nikizifanya kazi za Baba Yangu, basi ziaminini hizo kazi, kwa maana zinanishuhudia Mimi." Vivyo hivyo usiku wa leo.

161 Hebu tuichukue safu kwa safu. Ni kila mahali tu. Aminini sasa. Katika safu hizi hapa, ni wangapi hapo walio wagonjwa sasa, wanaojua ya kwamba siwajui? Inua tu mkono wako, useme, "Mimi ni mgonjwa, na—na—naomba, Mungu . . . "

162 Naangalia tu. Siwezi kulifanya litukie. Ni kama tu, siwezi kulielezea, ni kama ndoto tu, ni kwamba tu hu—hujalala. Ume—umejengwa, umezaliwa hivyo, kuona maono. Kama ningekwambia, "Niotee ndoto," usingeweza kufanya hivyo. Inahitaji mtu anayetengeneza . . . ambaye anakupa ndoto kulifanya. Siwezi kuona ono kwa ajili yako isipokuwa Mungu anionyeshe.

163 Laiti utakuwa na imani na kuamini kwamba niliyosema ni ukweli! Hivyo ndivyo alivyoniambia wakati Nuru hiyo iliposimama pale, ambapo wote walikuwa, kila mtu akiiangalia, walipozipiga zile picha. Iko Washington, DC, hatimiliki, Malaika wa Bwana. Wewe kuwa tu na imani ya kuamini.

164 Huyu hapa mwanamke. Sasa, ninawataka ninyi nyote, angalieni hapa. Hivi hamwezi kuiona hiyo Nuru inayoning'inia juu ya mwanamke huyu hapa, maskini mama anayeketi papa hapa nyuma? Sasa, hebu jaribu kuficha dhambi yako sasa. Ninatolea hilo changamoto kwa shindano la kuamua. Hivi hamwioni hiyo Nuru papa hapa? Sasa, angalieni kwa makini sana. Mwombe Bwana akuonyeshe, papa hapa: zumaridi, inayozunguka, ile ile . . . Ni wangapi wameiona picha Yake? Hebu tuuone mkono wako. Hakika. Vema, Hii hapa papa hapa. Mnaona, ni nini? Tuko katika kiwango fulani sasa.

165 Sijawahi kumwona mwanamke huyo. Lakini niangalie, Dada. Hatufahamiani. Sikujui wewe; Mungu anakujua. Ikiwa Bwana Yesu atanifunulia unachotaka, au jambo ambalo umefanya, jambo ambalo hukupaswa kufanya, au shida uliyo nayo, kitu ambacho unajua kwamba sijui lolote kukihusu, na kama anajua yaliyokuwako, kweli atajua yatakayokuwako, utajua kama hiyo ni kweli au la. Kama ataniambia hilo,

utaamini kuwa mimi ni mtumishi Wake na kuamini Uwepo Wake? Je, ninyi wengine mtaamini?

166 Mama huyu anaugua ugonjwa wa moyo. Hiyo ni kweli. Ana matatizo ya kibofu nyongo. Hivyo ndivyo daktari alivyomwambia. Sijawahi kumwona maishani mwangu. Hiyo ni kweli. Una mtu moyoni mwako unayemwombea. Ni mvulana, naye yuko kwenye huduma, wala hayupo hapa. Yuko mahali ambapo pana milima karibu: Denver. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Na anasumbuliwa na wasiwasi. Hiyo ni kweli. Je, unaamini Mungu anaweza kuniambia jina lako ni nani? Bibi Radcliffe. Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, mnaona ninachomaanisha na mwanaanga?

167 Sasa, hapa, kuna mtu anayevua miwani yake, akifuta machozi machoni pake. Anaivaa miwani yake tena. Nuru inaning'inia moja kwa moja kwake. Hatufahamiani. Anaugua ugonjwa wa yabisi kavu hata hivyo. Sikujui. Hatufahamiani. Je, hiyo ni kweli? Hutoki hapa. Unatoka Arkansas. Unaamini Mungu anaweza kuniambia jina lako, kama vile tu alivyomwambia Yesu jina la Petro ni nani? Bw. Vaughn. Hiyo ni sahihi. Rudi, ukiamini.

168 Huyu hapa mama mmoja ameketi papa hapa nyuma, akinitazama moja kwa moja. Hivi hamuioni hiyo Nuru juu ya mama huyo hapo? Hapo? Iangalieni. Mnaona? Hatufahamiani, lakini amemgusa. Anawasiliana. Amesogea moja kwa moja pale alipo, Roho wa Mungu. Mama huyu anaugua uvimbe titini mwake. Hiyo ni kweli. Hata yeye hatoki hapa. Umetoka Arkansas. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Bi. Sytack.

Mwanaanga!

Unamwombea mpendwa, sivyo? Yuna kansa. Dorothy Driscoll, um-hum, amini tu na uwe na imani. Itatukia. Um-hum.

Kivimbe kwenye titi, uvimbe. Bi Dickerson, kama utaamini kwa moyo wako wote, Mungu atakuondolea huo. Um-hum, um-hum, um-hum.

Simjui, sijawahi kumwona maishani mwangu. Hiyo ni kweli, sivyo? Mnaona ninachomaanisha? Mnaamini?

169 Mtaa wa Azusa kamwe haukuyaona mambo hayo. Hayo hayajakuwako, tangu Kristo alipokuwa duniani. Naye Kristo yuko duniani sasa katika umbo la Roho Mtakatifu katika Utimilifu Wake, akijaribu kuwatoa kwenye mambo haya ya ardhini, kuwainua katika Uwepo Wake. "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Je, mnaamini hayo?

170 Ni wangapi wenu mnaoshikilia kadi za maombi ili kuombewa? Ni wangapi kati yenu walio na imani na hawa ndugu wahudumu? Kuna wahudumu wangapi hapa? Inueni mikono yenu. Ningetaka baadhi yenu mje hapa, msimame

pamoja nami kwa muda kidogo, baadhi yenu ninyi ndugu mnaoamini katika uponyaji wa Kiungu.

171 Ninataka wale walio na kadi za maombi wapange mstari upande huu. Tutawaombea wagonjwa wakati upako huu unatenda kazi. Sitaki uondoke. Mnaona? Nataka kukuwekea mikono sasa hivi. Ninyi mlio na kadi za maombi, jipangeni papa hapa. Shukeni tu chini upande huu. Hebu baadhi ya wahudumu wa Injili waje hapa kwangu kwa muda kidogo tu.

172 Ukifa katika dhambi yako ya kutokuamini, Mungu hawajibiki. Kama ukifa katika dhambi yako ya kutokuamini, Mbele za Mwenyezi Mungu, ungewezaje kufanya jambo hilo?

173 Njoni hapa, ndugu wahudumu. Mhudumu yeyote anayetaka kuja kusimama pamoja nami, nina furaha kuwa pamoja na wewe. Wewe ni mwana wa Mungu. Njoo usimame pamoja nami unisaidie kuwaombea watu hawa wagonjwa. Njoni, ndugu. Simameni papa hapa wanapopanga mstari huu papa hapa.

(Billy, unaweza kushika kule chini? Kote pale hadi mwisho wa jengo.)

Ninyi mlio na kadi ya maombi sasa, simameni moja kwa moja kwenye marefu. Wengine, enyi kanisa, inamisha kichwa chako sasa katika maombi.

174 Ndugu wahudumu, je, mwaweza kuja moja kwa moja, upande wa pili kutoka hapa, karibu hapa, papa hapa karibu. Fanyeni miwili—mistari miwili, ili tuweze kuomba, kutoa nafasi.

Mungu wa Mbinguni awe pamoja nanyi hapa chini. Mungu wa Mbinguni . . .?. . .

175 Kila mtu pamoja sasa katika utakatifu mzito njoni kwenye marefu haya. Baadhi ya watu wenu watakuwa wamesimama katika mstari huu wa maombi. Kumbukeni, kwamba ikiwa Roho wa Kristo atafanya kazi za Kristo, na kama Roho wa Kristo amejithibitisha Mwenyewe sikuzote juma zima, katika wakati . . . Haijawahi kushindwa hata wakati mmoja. Wamishenari hawa hapa pamoja nami wanajua hilo. Nchi za kigeni, ambapo watu nusu milioni wamesimama, hata siwezi kuzungumza lugha yao, na kuwaambia vivyo hivyo: mambo ya kufanya, na wasiyopaswa kufanya.

176 Je, ni hao tu, ambao wataombewa? Sawa. Nyie wengine inamisheni vichwa vyenu sasa. Nami namtaka Don, tafadhali, aje hapa na kuongoza wimbo, *Tabibu Mkuu Sasa Yu Karibu*. Tafadhali msisogee isipokuwa unapitia kwenye mstari wa maombi. *Tabibu Mkuu*. Kila mtu inamisheni vichwa vyenu katika maombi.

177 Baba wa Mbinguni, sasa tunataka upako wa Roho, tunapoweka mikono yetu juu ya watu hawa wagonjwa. Na wapite hapa si kama wanapita karibu na ndugu zao, jalia

wapite huku wakijua kwamba Yesu Kristo yuko hapa katikati yetu, na tunatekeleza matakwa Yake na amri Zake tu.

178 Na iwe, Bwana, kwamba usiku huu, jalia kila mtu apitaye, na waponywe. Wabariki wahudumu hawa wa Injili hapa. Nguvu za Mungu na ziwe juu yao, na wanapotimiza agizo. . .

179 Maneno ya mwisho, Bwana, uliyotwambia ulipokuwa hapa duniani, ulisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: Kwa Jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; wakishika nyoka au kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Hilo ndilo ulilоahidi, Bwana.

180 Tuko hapa. Tuko katika wakati mgumu sana. Tuko katika majira magumu sana. Daima imekuwa hivyo dhidi ya ukweli wa Injili. Sasa, jalia litendeke usiku wa leo, Bwana. Jalia wale wasio na hatia, na wako tayari kuponywa, jalia waje na kuponywa, katika Jina la Yesu.

181 Sasa, wakati kanisa lote, kila mtu akiomba, mstari unapoingia, uwe katika maombi sasa. Nao, ndugu, wanapopita tu, ombeni, wawekeeni mikono yenu, kila mmoja akipita. Uondoke hapa ukimshukuru Bwana Yesu kwa uponyaji wako. Vema.

(Sawa, Don, tafadhali.) [Kusanyiko linaimba, *Tabibu Mkuu*. Maombi ya Ndugu Branham hayawezi kusikika—Mh.] . . .? . . .

182 Je, hao ndio wote waliopaswa kuombewa? Je, kuna mtu mwingine yeyote wa kuombewa? Ulikuwa mstari mfupi sana kwa ninii. . .Je, niliwaombea wote hivi majuzi usiku? Sawa. Wana watu kadhaa wanaoketi kwenye viti vya magurudumu. Tunataka kuwawekea mikono. Endeleeni tu kuimba na kuomba huku tukishuka kuwahudumia hawa.

[Kusanyiko linaimba, *Tabibu Mkuu*—Mh.] . . .? . . . [Mtu fulani anampa Ndugu Branham leso—Mh.] Imbeni zingine.

Katika Jina la Bwana wetu Yesu Kristo, jalia Roho Wako ashuke juu ya hawa, Bwana, na kuwaponya. Katika Jina la Yesu, ninaomba. Amina.

183 Hebu tusimame kwa miguu yetu sasa na kumsifu Mungu. Hebu—hebu tuinue mikono yetu na kusema, "Baba wa Mbinguni, kwa kufanya hivi tunakushukuru na kukusifu Wewe, kwa maana Wewe ndiwe Nguvu zetu. Wewe utusaidie, Bwana, na ufanye mambo haya kwa sababu Wewe ni Mungu na unalishika Neno Lako. Tunakupenda, na kukuheshimu, na kukusifu kwa moyo wetu wote."

Mungu, chukua ibada hii mikononi Mwako sasa. Mpe kila mtu imani, kupitia Jina la Yesu. Amina.

184 Shindilia nguzo yako chini sasa. Shindilia nguzo yako ya imani na kusema, "Papa hapa nalikubali. Hapa naliamini. Sasa hivi imekwisha. Naweza. Ninajua imekamilika, katika Jina la

Yesu Kristo.” Inueni mikono yenu, mpeni sifa, na kusema, “Asante, Bwana Yesu, kwa wema Wako.”

Vema, Ndugu Don. Um-hum. Mungu akubariki.

62-1125E Kuhesabu Kinyumenyume
Life Tabernacle
Shreveport, Louisiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


Voice Of God Recordings

P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

www.branham.org